

# Nia ya kuomba nafasi ya Mwaka wa 5 katika darasa la fursa

## Habari kwa waombajii wa mashambani/mbali

Mpendwa mzazi/mlezi

Madarasa ya fursa yanahudumia [wanafunzi wenye vipawa na uwezo wa juu](#) wa kiakili ambao wanaweza kuwa bila wanafunzi wenza wa kutosha katika cheo chao cha kitaaluma na kijamii.

Madarasa ya fursa yanatolewa katika Miaka ya 5 na 6, na wazazi/walezi wanatuma ombi katika Mwaka wa 4.

Darasa la fursa pepe la Mwaka wa 5 katika Aurora College linapatikana kwa wanafunzi wa mashambani na ya mbali ya NSW ambao watahudhuria shule za mwenyeji zilizoidhinishwa mwaka ujao.

Pakua orodha ya shule za mwenyeji zilizoidhinishwa hapa: <https://education.nsw.gov.au/content/dam/main-education/public-schools/selective-high-schools-and-opportunity-classes/media/oc-authorized-host-schools.pdf>

Wanafunzi wanaofaulu kupata nafasi katika Aurora College wanahudhuria shule yao ya umma ya eneo lao na kujiunga na darasa la fursa kwa masomo ya sayansi, teknolojia na hisabati kwa kutumia mfumo wa mikutano mtandaoni.

Wanafunzi kutoka shule ambazo sio za serikali ambao wamefaulu kupata nafasi watahitaji kujiandikisha katika shule ya umma kwenye orodha inayotajwa hapa juu, kama wakiishi katika eneo la shule. Maelezo zaidi juu ya darasa la fursa la Aurora yanapatikana kwa: <https://aurora.schools.nsw.gov.au/learning/primary-school.html>

## Upimaji na tathmini

Maombi kwa nafasi za darasa la fursa yanazingatiwa kwenye matokeo ya Mtihani wa Nafasi ya Darasa la Fursa peke yake. Wanafunzi wanaotaka kuzingatiwa kwa nafasi wanatakiwa kufanya Mtihani wa Nafasi ya Darasa la Fursa kwa tarehe inayoonyeshwa hapa kwenye ukurasa unaofuata wa mtandaoni

<https://education.nsw.gov.au/public-schools/selective-high-schools-and-opportunity-classes/general-information/key-dates->

## Jinsi ya kutuma ombi

Waombaji lazima waombe mtandaoni kati ya tarehe zinazoonyeshwa kwenye ukurasa wa tarehe muhimu kwenye <https://education.nsw.gov.au/public-schools/selective-high-schools-and-opportunity-classes/general-information/key-dates->

Fomu ya ombi inaweza kupatikana kwa <https://education.nsw.gov.au/oc>

Wazazi lazima watumie anwani yao ya barua pepe na sio anwani ya mtoto wao. Maombi yaliyochelewa kwa kawaida hayakubaliwi.

Wazazi wasiokuwa na upatikanaji wa mtandao wanaweza kuweka ombi katika maktaba ya umma. Ikiwa una ulemavu ambao hukuzuia kutumia kompyuta, unaweza kuwasiliana na Kitengo ili kupata usaidizi baada ya maombi yanapofungua.

**Muhimu:** Chagua 'Aurora College' kama chaguo lako la kwanza katika ombi la mtandaoni ikiwa unataka mtoto wako kuendelea katika shule ya sasa. Lazima uwasilishe ombi **moja** tu kwa kila mwanafunzi.

Fomu inayofuata **sio** ombi, bali ni ushauri kwa shule kwamba unakusudia kuweka ombi. Shule **haiwezi** kuweka ombi kwa niaba yako.

Mwaminifu wako

Mkuu

## Intention to apply for Year 5 placement in an opportunity class

For completion by rural/remote applicants

# Nia ya kuomba nafasi ya Mwaka wa 5 katika darasa la fursa

## Ili kukamilishwa na waombaji wa mashambani/mbali

### Hii sio ombi kwa kuingia darasa la fursa.

Hii ni notisi kwa shule yako ya msingi kwamba unakusudia kutuma maombi.

Ili kuweka ombi nenda kwa fomu mtandaoni kwa

<https://education.nsw.gov.au/oc>

*Tafadhali kamilisha habari hapa chini katika Kiingereza na irudishe kwa shule yako ya msingi.*

Jina la mwanafunzi

Darasa

Nakusudia kutuma ombi kwa nafasi ya Mwaka wa 5 mwaka ujao katika darasa la fursa kwa mtoto wangu. Nafahamu kwamba nahitaji kutuma ombi mtandaoni kati ya tarehe zinazoonyeshwa kwenye ukurasa wa tarehe muhimu kwa

<https://education.nsw.gov.au/public-schools/selective-high-schools-and-opportunity-classes/general-information/key-dates->

Jina la mzazi/ mlezi

(tafadhali andika vizuri)

Saini ya mzazi/mlezi

## Huduma ya mkalimani wa simu

Ikiwa unahitaji maelezo zaidi tafadhali upige simu kwa mkuu wa shule yako. Ikiwa unahitaji mkalimani ili kukusaidia na swali lako tafadhali upigie simu kwa Huduma ya Mkalimani wa Simu kwenye 131 450 na ulize kwa mkalimani katika lugha yako. Umwambie mpigaji simu nambari ya simu unayotaka kupigia simu, na mpigaji simu atapata mkalimani kwenye simu ili kukusaidia na mazungumzo. Hutatozwa kwa huduma hii.